**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA**

**SHULE YA SEKONDARI MKONO**

**S.L.P 475,**

**BUTIAMA,0755419792.**

**Mzazi/Mlezi…………………………..**
**S.L.P ………………………**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MKONO HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA MKOA MARA MWAKA 2024.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya HKL,HGLi,HGK, HGFa. **Hongera sana na karibu sana**.

MAHALI SHULE ILIPO
Shule ya Sekondari MKONO iko kata ya Bisumwa ,Wilaya ya Butiama ,Mkoa **wa** Mara umbali wa Kilometa 12 Magharibu mwa Mji wa MUSOMA

NAMNA YA KUFIKA SHULENI
Kwa wanaotoka Mikoani washukie Kituo cha Mabasi **Bweri** kilichopo Musoma mjini wachukue daladala hadi kituo cha daladala Musoma bus ulizia magari yanayoenda Bisumwa (Mkono sekondari) nauli ni sh 2000 na 4000 kwa pikipiki. Unashauriwa kufika Mjini kabla ya saa kumi na mbili jioni kuweza kuupata usafiri wa kuja shuleni

Muhula wa Masomo utaanza tarehe **08/07/2024** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **08/07/2024.** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **19/07/2024**

1. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni Suruali 2 rangi NYEUSI **ya kitambaa namba moja** (kitambaa kizito) yenye malinda 2 mbele. **ISIWE YENYE KUBANA. (MODO )**

ii. Mashati 2 ya tetron meupe yenye mikono mirefu. Mashati yanayobana hayaruhusiwi.



CamScanner

iii. Sare ya Michezo ni Kaptula na fulana yake nyekundu (jezi) kwa ajiri ya michezo isiye ya timu yeyote.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
v. Soksi jozi mbili nyeupe za shule.
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali
vii. Sweta la rangi ya samawati/ bluu lenye umbo la "v" shingoni (*taja rangi, idadi na mshono*) ; Inapatikana kwenye duka la shule
viii. Suruali mbili za kaki kwa ajiri ya kushindia (shamba dress)
ix. Tai rangi ya bluu yenye mistari myeupe (*inapatikana kwenye duka la shule,*);
x. Tisheti 02 rangi ya gold yenye nembo ya shule.(zina patikana kwenye duka la shule)
xi. Truck suit ya dark blue hii itamsaidia wakati wa baridi usiku na alfajiri. Inapatikana kwenye duka la shule

**1.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 07 ( counter book 4 quires);
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*).
iv. Godoro 1 la ft 3 x 6.
v. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue , blanket 1 ya kijivu, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya blue
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, mifagio 2 (mmoja soft broom na mmoja hard broom), dawa ya chooni lita 3. Na file mbili za spiring kwa matumizi ya kuhifadhia nyaraka zake shuleni.
x. Kadi ya BIMA ya afya ya NHIF au Tsh 51,000 kwa ajiri ya kutengenezea bima .
**xi. Taa Moja ya Solar hii itamsaidia pindi umeme utakapokatika.**

1.2 **Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango yote hiyo ilipwe kwenye account namba 30302301085 NMB yenye jina Self Reliance Mkono secondary. Unashauriwa kulipa popote kabla ya kufika Shule ili kuepuka usumbufu wa huduma za malipo ya kibenki.**

**TANBIHI: MALIPO YOTE YAFANYIKE KUPITIA BENK NA FEDHA TASLIMU HAZITAPOKELEWA. AJE NA HATI YA MALIPO TU IKIWA IMEANDIKWA JINA LA MWANAFUNZI.**



CamScanner

